



Toleo la miti TTS 16

Atriplex lentiformis, Jamii ya Chenopodiaceae

Atriplex lentiformis ni mti imara ulio wima wenye majani ya samawati-yanayong'ara na urefu wa 2cm. Mti huu hukua kwa haraka lakini wenye maisha mafupi ukilinganisha na aina nyingine ya miti katika jamii ya *Atriplex*. Majaribio kule Syria yalionyesha kwamba mti huu uliangamia baada ya kutimia umri wa miaka mitano. Mti huu waweza kuhimili viwango vya mchanga wenye chumvi, kuna ushahidi kwamba mti huu ulinawiri kwa kunyunyiziwa maji ya 100% kutoka kwa bahari kule Israeli. Mti huu pia huweza kuhimili viwango vya ukame na kunawiri katika sehemu kame. Mti huu hutekeleza jukumu kuu katika kurudisha hali muafaka ya sehemu kame na kwa kudhibiti mchanga katika miradi.

Jina la kawaida: Quail brush.

Maenezi: Mti huu ulitokea upande wa kusini Magharibi mwa USA na sehemu kame zenye joto kule Kusini mwa California na Arizona katika mwinuko wa chini. Mti huu umeenea katika sehemu kame za Australia na Iran. Mti huu umeanzishwa na kufanyiwa majaribio katika visiwa vya Cape Verde na shirika la HDRA.

Mazingira

Mvua: 300-450mm, katika majaribio ya Cape Verde mwaka wa 1989 mti huu uliweza kunawiri katika viwango vya mvua ya 111mm ambayo ilinyesha tu kwa siku 9.

Kiwango cha joto: Viwango vya 18.6-27.7 °C vilishuhudiwa kule Cape Verde. Mti huu waweza kuhimili theluji, hata hivyo hufanya vyema katika hali za kadri.

Mwinuko: Mwinuko wa nyanda za chini.

Aina ya mchanga: Hufanya vyema katika mchanga wa chumvi.

Ukuaji

Urefu: 2.5m.

Kipenyo cha shina:

Kilele: huenea kwa wingi sana.

Maua: *A. lentiformis* ni mmea ulio na maua kwenye miti miwili tofauti. Maua ya kiume yapo kwenye chana lililo kwenye matawi ili hali yale ya kike huning'inia katika makundi.

Tunda: Tunda hili ni jembamba na la mviringo na kipenyo cha 2.5mm.

Matumizi

Matumizi ya maana: Uwezo wa mti huu katika kuhimili chumvi hufanya kuwa bora zaidi katika kuimarisha maeneo yenye ukame. Mti huu hutumiwa kwa wingi kama lishe la kondoo na hasa katika nchi ya Australia. Hata hivyo, iwapo mmea huu utatumiwa kwa wingi kama lishe, basi kondoo watahitaji maji mara tatu zaidi ya kiwango cha kawaida. Hali hii yaweza kukabiliwa kwa kuambatanisha mseto wa mimea yenye majimaji kama vile *cactus*.

Mengine: Utafiti umebainishwa kwamba mti huu waweza kuwa kivuli kwa mimea mingine inayostahimili chumvi. Kule Cape Verde, kwa mfano, utafiti umefanywa ili kutumia mti huu kama kivuli cha jamii ya miti ya *Sesbania* katika nyanda za pwani.

Maelezo ya upanzi

Panda moja kwa moja kutoka kwa mbegu au kwa kutumia kiunga kisha kuatika. Waweza pia kutumia vipandikizi.

Matayarisho kabla ya upanzi: Kabla ya kupanda, osha mbegu ili kuondoa chumvi. Kuloweka mbegu hupunguza muda wa kuota kwa kiasi kikubwa.

Ukuaji: Licha ya kwamba *A. lentiformis* ni mmea unaofanya vyema katika maeneo ya chumvi, kiwango kikubwa cha chumvi chaweza kuathiri ukuaji wa mmea huu, Hivyo basi ni bora kupanda katika kiunga.

Kiunga: Panda kwenye trei na kisha kuatika kwa vifuko.

Utunzaji: Atika miche kwingineko punde inapotimia urefu wa 20-30cm baada ya miezi 3-6. Kata kwa kimo kitakacho ruhusu mifugo kutafuna majani.

Mengine

Upungufu: Iwapo mmea huu utatumiwa kama lishe la mifugo, basi maji ya kunywa yapaswa kuwepo kutokana na kiwango kikubwa cha chumvi. Hali hii yaweza kukabiliwa kwa kupanda aina ya lishe lingine lenye maji mengi kama *cactus* ili kukidhi hitaji la maji.

Tafsiri na;

Patrick Bunyali Kamoyani- Maragoli, Kenya

Simu: +254-0-721 612 607

Barua-pepe: pbkamoyani@excite.com au pbkamoyani@lycos.co.uk

Produced by The Tropical Advisory Service, December 2002. This translation May 2007

HDRA - the organic organisation, Ryton Organic Gardens Coventry, CV8 3LG, UK.

Tel: +44(0)24 7630 3517 Fax: +44(0)24 7663 9229 Email: ove-enquiry@hdra.org.uk

<http://www.hdra.org.uk>

Makala haya ni mkusanyiko wa utafiti wa Kisayansi na maelezo kutoka kwa wakulima aina mbalimbali.

Orodha ya marejeleo na majarida mengine muhimu yaweza kupatikana katika shirika la HDRA. Makala haya yanaweza kunakiliwa bure kwa shughuli zisizo za kibiashara.